# TIBA YA KUTIKISA KUPITIA STIMA KWA WAGONJWA WALIOZUILIWA HOSPITALINI

(Sehemu ya 58A ya Sheria ya Afya ya Akili 1983)

## Je! kijikaratasi hiki kinahusu nini?

Kijikaratasi hiki kinafafanua sheria maalum katika Sheria ya Afya ya Akili ya 1983 kuhusu utumiaji wa tiba ya kutikisa kupitia stima (ECT) kutibu shida ya akili. Sheria hizo ziko katika sehemu ya 58A ya Sheria ya Afya ya Akili.

## Je! tiba ya kutikisa kupitia stima ni nini?

ECT in matibabu yanayotumiwa kwa idadi ndogo ya shida kali za akili, kama unyogovu mkali, wazimu mkali na katatonia. Wakati wa ECT, mkondo wa umeme hupitishwa kwa muda fupi kwa ubongo, ambayo husababisha mshtuko wa moyo (‘ugonjwa wa ghafla wa muda mfupi’). ECT hupewa chini ya nusukupati ya jumla na wagonjwa pia hupewa madawa ya kutuliza misuli yao ili kuzuia wao kujiumiza wakati wa ugonjwa wa ghafla wa muda mfupi. Kawaida, ECT hupewa katika kozi ya vikao sita au 12, na wafanyikazi waliofunzwa kwa njia maalum.

Ikiwa wafanyikazi wa hospitali wanafikiria kuwa itakuwa wazo nzuri wewe kupata Tiba ya ECT, watakuelezea ni nini, na ni lini wanafikiria unapaswa kupata.

## Je! ninaweza kukataa ECT?

Ikiwa unaweza kujiamulia wewe mwenyewe, sio lazima ukubali ECT ikiwa hauitaki. Utapewa tu ECT ikiwa utakubali, au ikiwa ni dharura.

## Je! na ikiwa niko chini ya miaka 18?

Ikiwa una umri wa chini ya miaka 18 na unakubali ECT, daktari ambaye hatoki kwenye hospitali ambapo unatibiwa atakuja kukuona.

Daktari huyu wa kujitegemea anaitwa SOAD (Daktari wa Maoni ya pili aliyewekwa) (Second Opinion Appointed Doctor) na ameteuliwa na Tume inayojitegemea ambayo inaangalia jinsi Sheria ya Afya ya Akili inatumika.

Daktari huyu wa kujitegemea atazungumza nawe na wafanyikazi katika hospitali wanaokujua.
Unaweza tu kupewa ECT ikiwa wewe na daktari wa kujitegemea mmekubaliana nayo, au ikiwa ni dharura.

## Je!  na ikiwa wafanyikazi wa hospitali wanafikiria sina uwezo wa kujiamulia mimi mwenyewe?

Wafanyikazi wa hospitali wanaweza kufikiria kuwa, kwa sababu ya shida yako ya akili, hauwezi kujiamulia mwenyewe kama utapata ECT.

Hii inamaanisha wanafikiria hauwezi kuelewa ECT ni nini, ni ya nini, na athari zake ni nini na manufaa yake yanaweza kuwa nini.

Ikiwa wanafikiria hauwezi kujiamulia wewe mwenyewe, wafanyikazi wa hospitali watamuuliza daktari wakujitegemea (SOAD) aje akuone. Daktari huyu wa kujitegemea atazungumza nawe na wafanyikazi katika hospitali wanaokujua.

Ikiwa daktari wa kujitegemea atakubali kuwa wewe hauwezi kujiamulia wewe mwenyewe, daktari wa kujitegemea anaweza kukubali kuruhusu wafanyikazi wa hospitali wakupe ECT. Isipokuwa ni hali ya dharura, unaweza tu kupewa ECT ikiwa daktari wa kujitegemea amekubali.

Lakini daktari wakujitegemea hawezi kukubali kuruhusu wafanyikazi wa hospitali wakupe ECT ikiwa umefanya uamuzi wa mapema unaofungwa kisheria kukataa ECT chini ya Sheria ya Uwezo wa Kiakili 2005, au mtu mwingine anayeruhusiwa kufanya uamuzi kwa niaba yako chini ya Sheria hiyo amesema kuwa haupaswi kuipata. Huyu anaweza kuwa mtu ambaye umempa uwezo wa wakili wa kudumu, makamu aliyeteuliwa kwako na Korti ya Ulinzi, au Korti ya Ulinzi yenyewe. Wafanyikazi wa hospitali wanawezakupa habari zaidi kuhusu Sheria ya Uwezo wa Kiakili 2005.

## Je! ni nini hufanyika wakati wa dharura?

Katika hali ya dharura, unaweza kupewa ECT hata ikiwa wewe au daktari wa kujitegemea hamjakubali.

Lakini hii inaweza kufanywa ikiwa unahitaji kupewa ECT mara moja ili kuoka maisha yako, au kuzuia afya yako ya akili kuwa mbaya zaidi.

## Kanuni za Kufanya kazi

Kuna Kanuni za Kufanya kazi zinazotoa ushauri kwa wafanyikazi hospitalini kuhusu Sheria ya Afya ya Akili na kutibu watu walio na shida ya akili. Wafanyikazi wanapaswa kuzingatia Kanuni inasema nini wakati wanapofanya uamuzi kuhusu utunzaji wako. Unaweza kuuliza nakala ya Kanuni, ikiwa unataka.

## Ninapaswa kulalamika aje?

Ikiwa unataka kulalamika kuhusu jambo lolote linalohusiana na utunzaji wako na matibabu katika hospitali tafadhali ongea na mfanyikazi. Hii inaweza kusaidia kutatua swala hilo. Wanaweza kupa habari kuhusu utaratibu wa malalamishi ya hospitali, ambayo unaweza kutumia kujaribu kutatua malalamishi yako kupitia jambo linaitwa suluhisho za kawaida. Wanaweza pia kukuambia kuhusu watu wengine wowote ambao wanaweza kukusadia kulalamika.

Ikiwa hauhisi kuwa utaratibu wa malalamishi ya hospitali unweza kukusaidia, unaweza kulalamika kwa Tume ya Kujitegemea. Tume hiyo huchunguza jinsi Sheria ya Afya ya Akili inatumika, kuhakikisha inatumiwa vyema na kuwa wagonjwa wanatunzwa vyema wakiwa hospitalini. Wafanyikazi wa hospitali wanaweza kukupa kijikaratasi kinachofafanua jinsi ya kuwasiliana na Tume.

## Usaidizi na habari zaidi

Ikiwa kuna jambo lolote ambalo hauelewi kuhusu utunzaji wako na matibabu yako, wafanyikazi watajaribu kukusaidia. Tafadhali uliza mfanyikazi kukufafanulia ikiwa kuna jambo lolote katika kijikaratasi hiki ambalo hauelewi au ikiwa una maswali mengine ambayo kijikaratasi hiki hakijajibu.

Tafadhali uliza nakala nyingine ya kijikaratasi hiki ukitaka kumpa mtu mwingine.